

3SquaresVT

*Mradi wa Vermont wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada
(Vermont's Supplemental Nutrition Assistance Program)
(ilikuwa ikiitwa Food Stamps)*

Maswali na Majibu kwa Wahamiaji

Nitakuwa na shida ya kupata kadi yangu ya kijani nikipokea marupurupu ya 3SquaresVT?

La. Kupata marupurupu ya 3SquaresVT au usaidizi mwingine usiokuwa wa kifedha hautakuharibia unapofanya maombi ya kadi ya kijani.

Mtoto wangu anaweza kupata marupurupu ya 3SquaresVT hata kama mimi sistahili?

Ndio. Hata kama huna hati sawa au wewe mwenyewe huwezi kupata marupurupu ya 3SquaresVT, mtoto wa chini ya miaka 18 anayeishi hapa kihalali anaweza kupata marupurupu. Ukifanya maombi ya 3SquaresVT kwa niaba ya mtoto wako, hautahitajika kupeana namba yako ya hazina ya jamii (social security) au kujibu maswali kuhusu hali yako ya uhamiaji. Hata hivyo, utahitaji kupeana maelezo kuhusu mapato yako na malimbiko yako.

Nikifanya maombi ya 3SquaresVT, watu wanaoishi na mimi watatakiwa wajibu maswali kuhusu hali yao ya uhamiaji?

Ni wale tu wanaotaka kupokea marupurupu ya 3SquaresVT ndio wanatakiwa kujibu maswali kuhusu hali yao ya uhamiaji. Watu wanaoishi kwenye nyumba hiyo na hawataki marupurupu ya 3SquaresVT hawatahitaji kuonyesha hati zozote zauhamiaji ama kupeana namba zao za hazina ya jamii (social security) lakini watahitaji kupeana maelezo kuhusu mapato yao na malimbiko yao.

Idara ya Huduma ya Kiuchumi kwa Watoto na Jamii [Department for Children and Families Economic Services Division] (ESD) itaniripoti kwa Idara ya Uhamiaji na Forodha [ICE (Immigration & Customs Enforcement)] kama nitakataa kujibu maswali kuhusu hali yangu ya uhamiaji?

La. Kama hutaki kujibu maswali kuhusu hali yako ya uhamiaji, DCF na ESD hawatakiwi kukuuliza maswali yoyote ya ziada au kujaribu kufahamu zaidi kuhusu hali yako ya uhamiaji kutoka kwa mtu yeyote. Hawatakuripoti kwa ICE. Hata hivyo, kama wana thibitisho kuwa hauna hati, basi wanapswa kukuripoti kwa ICE.

Naweza kupata mtafsiri anisaidie kufanya maombi ya marupurupu ya 3SquaresVT?

Ndio. Kama unahitaji mtu akusaidie kuwasiliana na mhudumu wako wa DCF/ESD, unaweza kuomba mtafsiri, na ESD itamlipa.

Nilifanya mambo ya 3SquaresVT na nikanyimwa. Nifanyeje?

Kama wafikiria unastahili kupata marupurupu ya 3SquaresVT, unaweza kukata rafa ya uamuzi wa ESD. Ni lazima ufanye maombi ya rufani kabla siku 90 kwisha kwa kuandikia au kupigia simu ofisi ya ESD (no bora kuwaandikia). Vermont Legal Aid au Legal Services Law Line wanaweza kukupatia wakili au msaidizi wa kisheria uongee naye.

**Kama unahitaji usaidizi au una maswali, tafadhali piga simu
Vermont Legal Aid kwa 1-800-769-7459.**



*Ujumbe huu umedhaminiwa kwa kiasi na USDA,
Mpena nafasi tena muajiri kwa usawa.
4/10/09*

